Bahati Binti Mfalme

Mtunzi: Deogratias Simba
Mchoraji: Michael Sagikwa

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 1 6/16/23 15:31

Bahati aliishi katika nchi ya Susu.
Alikuwa binti wa mfalme.
Wazazi wake walikuwa watawala wa Susu.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 2 6/16/23 15:31

Mvua haikunyesha kwa muda. Nchi ya Susu
ilikabiliwa na ukame kwa muda mrefu.
Watu hawakuwa na chakula wala maji.
Mimea ilikauka. Wanyama walitaabika bila maji.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 3 6/16/23 15:31



Taabu za wanasususu zilifika kwa mfalme. Mfalme na washauri waliwaza wafanye nini. Waliitisha kikao kujadili hali ile.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 4 6/16/23 15:32

Bahati alipenda kukaa karibu na baba yake mfalme wa Susu. Alihudhuria vikao alivyofanya mfalme na washauri wake.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 5 6/16/23 15:32

Mfalme alipojadili tatizo la ukame na washauri wake, Bahati naye aliwaza afanye nini kutatua matatizo ya nchi ya Susu.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 6 6/16/23 15:32

Bahati alipata wazo.
Alitaka kumwambia baba yake, lakini hakumpa nafasi kwa sababu Bahati alikuwa mdogo sana.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 7 6/16/23 15:32

Bahati alikwenda kwa mama yake, ambaye alikuwa malkia wa Susu. Malkia alimsikiliza na kuahidi kumsaidia.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 8 6/16/23 15:32

Malkia alikwenda kwa mfalme na washauri wake. Aliwasihi wasikilize wazo la Bahati.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 9 6/16/23 15:32

Mfalme wa Susu alimpa Bahati nafasi ya kuongea mbele ya washauri. Bahati alisimama mbele ya baraza lile na kueleza wazo lake.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 10 6/16/23 15:32

Aliwaeleza watu wa Susu wazuie maji ya mvua. Wasiyaache yote yaelekee mtoni. Kisha wachimbe bwawa la kuyahifadhi.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 11 6/16/23 15:32



Pia wazuie maji ya mto na kuyaelekeza bwawani.
Maji ya bwawani yatawasaidia hasa kipindi cha ukame.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 12 6/16/23 15:32



Mfalme na washauri walifurahishwa na wazo la Bahati. Walipanga kuwaeleza wananchi wa Susu ili walitekeleze.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 13 6/16/23 15:32

Bahati aliwaongoza vijana wa Susu su. Walichimba bwawa kubwa. Wengine walichimba mifereji kuelekea bwawani.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 14 6/16/23 15:32

Mvua ziliponyesha, mifereji ilipeleka maji bwawani. Mto nao ulitiririsha maji bwawani. Bwawa lilikuwa na maji ya kutosha.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 15 6/16/23 15:32



Maji yalifika Susu.
Watu walipata maji. Mimea ilinyeshewa. Wanyama walipata majani na maji. Bahati, Mfalme, malkia na watu wote wa Susu walifurahi sana.

TZ-LLP-15-0007_Text_PrincessBahati.indd 16 6/16/23 15:32